NIPASHE UK 11



# Vijana kunufaika uvuvi na mifugo

**Na Allan Isack, ARUSHA**

VIJANA kutoka mikoa 13 ya Tanzania watanufaika na mtandao wa vijana unaojihusisha na shughuli za uvuvi na mifugo ili kujikwamua kiuchumi.

Lengo la kuanzishwa kwa mtandao huo ni kutawasaidia vijana kujiajiri kupitia shughuli za uvuvi na mifugo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mtandao huo uliofanyika jijini hapa, Rais wa Mtandao huo, Laban Boaz, alisema vijana chini ya umri wa miaka 35 kutoka mikoa hiyo, watanufaika na mtandao huo, kwa kufundishwa mbinu bora za kisasa za ufugaji na uvuvi.

Boaz alisema lengo la kuanzishwa kwa mtandao huo ni kuhamasisha vijana kujiajiri katika sekta za mifugo na uvuvi kwa kutumia njia za kisasa ambazo zitasaidia kuongeza uzalishaji mali na ajira kwa vijana.

Rais huyo alisema walianzisha mtandao huo baada ya kuona kuwa kuna mwanya wa kimaendeleo kati ya wazee na vijana .

"Mtandao huu utasaidia kuwapa ujuzi na maarifa vijana namna ya kufuga kisasa, na vijana waliopo vijijini ambao hawakupata maarifa ya mtandao huu watanufaika wote," alisema Boaz.

Alisema mtandao huo, ulianzishwa jijini Dar es Salaam mwaka 2017 lengo likiwa kupanua wigo kwa vijana nchini.

Mkurugenzi wa Uzalishaji na Masoko wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Felix Nandonde, alisema mtandao huo ni juhudi za muda mrefu zilizofanywa na Umoja wa Afrika kupitia mradi wa kuendeleza rasilimali za wanyama (AU-IBAR) .

Aidha, alisema mtandao huo, umewashirikisha vijana wanaojihusisha na kazi tofauti katika mnyororo wa dhamani ya mifugo, samaki, kuku na nguruwe ambapo vijana hao kupitia mtandao huo watawekwa pamoja na kufanya kazi ya mnyororo wa thamani.

Nandonde alisema serikali itaendelea kushirikiana na mtandao huo, kuwafikia vijana ili waitumie fursa hiyo ipasavyo.

Scanned by CamScanner

FURSA

MTANZANIA UK IV

# Fursa sekta ya maziwa imepewa kisogo, ukuaji unasuasua



**Inatoka i**

Anafafanua zaidi kuwa fursa hizo ni uwekezaji katika kuzalisha, kusafirisha na kuuza vyakula vya mifugo ambazo bado hazijafanyiwa kazi na kuchangamkiwa kikamilifu.

Anabainisha fursa nyingine kuwa ni ile ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa ikiwa ni pamoja na uzalishaji wake.

"Ni bayana kwamba Tanzania tumebarikiwa kuwa na mifugo mingi hasa ng'ombe wakiwamo wale wa maziwa, lakini changamoto inakuja kwamba bado fursa zilizoko huku hazichangamkiwi kikamilifu, hatua ambayo inailazimu nchi kuagiza maziwa kila mwaka.

"Lakini ukiacha hiyo, fursa nyingine ni kuanzisha viwanda vya usindikaji, usafirishaji, kuuza maziwa na bidhaa zake, kuwekeza katika mashine za kusindika na magari ya kusafirishia," anasema Dk. Sophia.

Anasema fursa zote hizo bado hazijafanyiwa kazi ipasavyo jambo linalosababisha sekta ya maziwa kukua kwa kusuasua.

Aidha, Dk. Sophia anasema lipo pengo kubwa kati ya kiwango cha maziwa kinachozalishwa nchini na unywaji wa maziwa.

Anasema kwa sasa inakadiriwa kuwa Mtanzania anakunywa lita 49 tu kwa mwaka tofauti na inavyoshauriwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kunywa angalau lita 200 kwa mwaka.

Anasema kwasasa viwanda vinavyosindika maziwa nchini vipo 99 vyenye uwezo wa kusindika lita 500 hadi 100,000 kwa siku, kwa kila kimoja.

Hata hivyo, viwanda vikubwa vipo sita vyenye uwezo wa kusindika lita 194,335 kwa siku na kwa mwaka lita milioni 70, kiwango ambacho kinasuasua kutokana na uhaba wa malighafi.

"Pamoja na kiwango hicho, uwezo wa uzalishaji katika viwanda hivyo vikubwa ni kusindika lita 862,000 lakini kutokana na uhaba wa malighafi vimelazimika kusindika chini ya hapo.

"Bado kuna mazao ya maziwa ambayo hayazalishwi nchini kama maziwa ya unga jambo linalosababisha uagizaji wa bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi ili kumrahisishia Mtanzania kupata bidhaa anayohitaji.

"Hivyo, kama bodi tumejiwekea mikakati ya kuongeza uzalishaji na uchakataji wa maziwa nchini ili kukidhi mahitaji ya soko na ustawi wa jamii yenye afya," anasema Dk. Sophia.

Anaainisha mikakati hiyo kuwa ni pamoja na ule wa kuongeza idadi ya ng'ombe wa maziwa kutoka milioni 1.3 waliopo sasa hadi kufikia milioni tatu.

"Katika hili tumejipanga kuongeza uzalishaji wa ng'ombe kupitia uzalishaji kwa njia ya chupa (Artificial Insemination) pamoja na ule wa njia ya kutoa ndama wengi kwa wakati mmoja (Embryo Transfer).

"Ongezeko hili la idadi ya ng'ombe wa maziwa litasaidia kuongeza wingi wa maziwa yanayozalishwa hadi kufikia lita bilioni saba.


"Mkakati huu utakwenda sambamba na kuhakikisha upatikanaji wa malisho na chakula cha ng'ombe hao kinapatikana kwa kila mkulima kuwa na shamba la malisho," anasema.

Dk. Sophia anasema ili kuondoa magonjwa yatokanayo na wadudu wa mifugo, serikali imetoa ruzuku kuimarisha majosho nchini kwa kuwaogesha ng'ombe wote.

Anasema kila ng'ombe ataogeshwa kwa gharama ya Sh 50 fedha ambayo hubaki kwa wafugaji ili kusaidia kuongeza dawa inapopungua katika majosho.

Anasema mkakati mwingine ni kuwakusanya wafugaji na kuwaunganisha katika vikundi ili waweze kusaidiwa na taasisi za fedha.

"Tumehamasisha vikundi vya ushirika 19 vyenye wajumbe 3,232 ambao wamepewa mafunzo ya namna ya kuzalisha kusafirisha na kusindika maziwa na bidhaa zake.




"Vikundi viwili vya mkoani Tanga ambavyo ni Chaumu kilichopo Muheza na Uwamwa cha Lushoto vilipatiwa fedha kutoka Benki ya Kilimo (TADB) ambapo Chaumu kilipata Sh milioni 142.242," anasema Dk. Sophia.

Anasema wanaendelea na uhamasishaji wa wawekezaji ambao watawekeza katika sekta ya maziwa ili kuongeza kiwango cha maziwa yanayochakatwa.

Anasema pia wanaendelea na uhamasishaji wa unywaji maziwa ikiwa ni pamoja na kuwa na bonanza la maziwa, wiki ya maziwa na siku ya unywaji maziwa shuleni.

Anasema changamoto ni kwamba wafugaji wamesambaa nchini kote hivyo, inakuwa vigumu kukusanya maziwa na kuyapeleka viwandani.

"Tumeamua kujenga kituo cha kukusanyia maziwa cha mfano katika Wilaya ya Mkuranga, kitakachokabidhiwa kwa chama cha ushirika kiweze kuendeshwa.

"Kwa kushirikiana na sekta binafsi ya Heifa International, tunajenga vituo vingine 10 ambapo vitatu vitakuwa na uwezo wa kupokea lita 5,000 kila kimoja, vituo sita lita 3,000 kila kimoja na kimoja lita 2,000," anabainisha Dk. Sophia.

Anasema wamekubaliana na kiwanda cha ASAS kujenga vituo vya kukusanya maziwa 40 katika Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya.

Anaongeza kuwa vituo vingine sita pia vitajengwa kwa kushirikiana na shirika la COPE kutoka Italia katika Mkoa wa Ruvuma.

"Vituo saba vya kukusanyia maziwa vitajengwa kwa kushirikiana na Propherty Investment katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani," anasema Dk. Sophia.

Anasema hadi kukamilika kwa mwaka huu wa fedha wanatarajia kukamilika kwa vituo vya kukusanyia maziwa 54.

Hata hivyo, anasema bado kuna changamoto nyingi katika uwekezaji wa sekta ya maziwa zikiwa ni pamoja na maziwa kuwa ni zao linaloharibika haraka hivyo linahitaji kuchakatwa haraka.

Anasema miundombinu iliyopo haisaidii kuwahi kusafirisha maziwa kwenda katika viwanda vya uchakataji.

"Bado elimu ya unywaji maziwa yaliyosindikwa haijaifikia jamii jambo ambalo linasababisha wengi kuchemsha nyumbani bila kuwa na vipimo vya kupimia kama yamekuwa salama," anasema Dk. Sophia.

Anasema changamoto nyingine ni viwanda vingi havijaweza kuzalisha bidhaa nyingi zitokanazo na maziwa japo kuwa kuna viwanda vimeanza kusindika maziwa yanayoishi muda mrefu bila kuharibika.

Anaongeza kuwa bado Watanzania wengi hawazijui bidhaa nyingine zitokanazo na maziwa jambo linalosababisha baadhi ya bidhaa kukosa soko.

Anasema jambo lingine ni bidhaa nyingi zinazosindikwa zinapatikana mjini pekee huku maeneo ya vijijini hawapati hivyo kulazimishwa kunywa maziwa yasiyosindikwa.

Dk. Sophia anatoa wito kwa Watanzania kuwekeza katika tasnia ya maziwa katika mnyororo wa kuongeza thamani.

"Kuna faida kubwa katika mnyororo wa kuongeza thamani maziwa kuanzia kuzalisha chakula, kufuga, kutengeneza keni za kusafirishia maziwa, kusindika, kusafirisha na kuuza," anasema Dk. Sophia.

Anawaomba Watanzania kila mmoja kuhakikisha anakunywa maziwa yaliyosindikwa glasi moja kila siku kwa ajili ya afya bora.

"Niwaombe wote wanaojihusisha na uwekezaji katika mnyororo wa kuongeza thamani maziwa kujisajili TDB ili ajengewe uwezo wa biashara hiyo," anasema Dk. Sophia.

Dk. Sophia anawashauri wote wanaojihusisha na biashara ya maziwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza sekta hiyo.

"Nawakaribisha wadau wa maziwa na wananchi kwa ujumla kushiriki katika wiki ya maziwa itakayofanyika Dodoma, Mei 28, hadi Juni Mosi, mwaka huu.


"Waje kushiriki kuonesha bidhaa zao, kujifunza teknolojia mpya ya ufugaji bora, pia waje kunywa maziwa na mazao yake," anasema Dk. Sophia.

Scanned by CamScanner

UFUGAJI

MTANZANIA UK 11

# *Fursa sekta ya maziwa imepewa kisogo, ukuaji unasuasua*



Na TUNU NASSOR

TANZANIA imebarikiwa kuwa nchi yenye fursa nyingi lakini jambo la kushangaza ni kwamba bado Watanzania hawajazitumia ipasavyo katika kuwaletea kipato.

Kama ulikuwa hufahamu ni kwamba Tanzania inashika nafasi ya pili barani Afrika kwa kuwa na mifugo wengi ikitanguliwa na Ethiopia.

Kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa sasa Tanzania ina ng'ombe zaidi ya milioni 32.5, mbuzi milioni 18.8, kondoo milioni 5.3, nguruwe milioni 1.9 na kuku milioni 38.8.

Aidha, kati yao, ng'ombe wa maziwa ni 1,294,882 ikilinganishwa na Kenya ambayo ina milioni 4.2.

Hata hivyo, pamoja na kuwa na mifugo hiyo, bado inazalisha lita bilioni 2.7 za maziwa kila mwaka huku Kenya ikizalisha lita bilioni 5.2.

Pamoja na kuzalisha kiwango hicho cha maziwa, bado viwanda vya maziwa vinachakata asilimia 34 tu ya maziwa yazalishwayo nchini, hivyo kuwaacha wakulima wakiendelea kukabiliwa na hali ngumu ya maisha kutokana na kukosa soko la uhakika la maziwa yao.

Kutokana na hali hiyo, Tanzania inalazimika kuagiza maziwa na mazao yake lita milioni 20 kutoka nje ya nchi kwa kutumia zaidi ya Sh bilioni 50 kila mwaka.

Dk. Sophia Mlope, ni Msajili wa Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB), anazungumzia hali ya uzalishaji wa maziwa nchini akisema kuwa kuna fursa nyingi ambazo hazijapata uwekezaji katika sekta ya maziwa ambazo iwapo zikifanyiwa kazi zinaweza kuongeza uzalishaji.

Inaendelea Uk.iv

**KILIMO** Suluhu mboga mboga kuozea shambani - UK v

Scanned by CamScanner